REPUBLIQUE DU BURUNDI

SENAT

ASSEMBLEE NATIONALE

PRESIDENT

Réf : SNB/CP/...436.../2021

Réf : 130/PAN/...009.../2021

Bujumbura, le 20/12/2021

**TANGAZO LA BUNGE NA SENETI ZA JAMHURI YA BURUNDI BAADA YA KIKAO MAALUM CHA DESEMBA 20, 2021 KILICHOFANYIKA KATIKA JUMBA LA MIKUTANO LA KIGOBE.**

**INAHUSU: RIPOTI YA MAENDELEO KIHATUA KUTOKA TUME YA UKWELI NA MARIDHIANO, MWAKA WA 2021**

**Bunge la Taifa na Seneti za Jamhuri ya Burundi zikikutana katika kikao maalum;**

- **Kufuatia** Katiba ya Jamhuri ya Burundi, hasa katika kipengele chake cha 168, pointi ya 8;
- **Kuchukulia** sheria iliyorekebishwa n°1/22 ya Novemba 6, 2018 inayolenga uundwaji, mamlaka, utungwaji, mpangilio na utendaji kazi wa Tume ya Ukweli na Maridhiano (CVR), hasa katika kifungu chake cha 69 kinachotarajia "kwamba "**Tume ya Ukweli na Maridhiano inatoa ripoti ya maendeleo kihatua kila mwaka kupitia kikao maaluum cha Bunge na Seneti kwa pamoja** ";

**A. Kwa kuzingatia** ripoti ya maendeleo kihatua iliyowasilishwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano tarehe 20 Desemba 2021;

Sénat
Avenue du Peuple Murundi
B.P. 114 GITEGA-BURUNDI
Tél : (257) 22 40 50 08 – 22 40 5 023
E-mail : cabinet@senat.bi – senat@senat.bi
Site Web : www.senat.bi

Assemblée Nationale
B.P. 120 BUJUMBURA-BURUNDI
Tél : (257) 22 26 70 11
Fax : (257) 22 26 70 12
E-mail : assemblenationale_burundi@yahoo.fr

**B. Kwa kuzingatia** mfumo uliotumiwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano katika kazi yake ya kubainisha ukweli kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kwa nia ya kuchunguza njia za upatanisho wa Wanaburundi na kutoripotiwa tena kwa uhalifu uliotendwa myaka ya 1972 na 1973;

**C. Kukubaliana na kwamba** sampuli ya ufukuaji wa makaburi ya halaiki, vikao vya mashahidi na kumbukumbu ambazo tayari zimekusanywa na kufanyiwa mtazamo ni uthibitisho sahihi na tosha;

**D. Baada ya kuchambua** magubiko ya ripoti ya hali ilivyoendelea sawa na maandalizi yake upande wa Tume ya Ukweli na Maridhiano;

**E. Baada ya kutathmini** majukumu yaliyokabidhiwa kwa Tume ya Ukweli na Maridhiano, yenye dhamira hasa ya:

- Kufafanua ukiukwaji wa haki kuu za kisiasa, kiraia, kiuchumi na kijamii;

- Kudhihirisha wajibu wa mtu binafsi na ile ya taasisi za serikali, watu wa kisheria na vikundi vya kibinafsi;

- Kuonesha vizuri nafasi ya mkoloni katika vurugu za mzunguko ambazo ziliathiri Burundi;

- Kubainisha asili, sababu na kiwango cha vitendo vya ukiukaji vilivyofanyika, ikiwa ni pamoja na yaliyotangulia, hali kimazingira, mambo hasa, miktadha, lengo na mitazamo iliyosababisha ukiukaji huu;

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P. 120 BUJUMBURA
ASSEMBLEE NATIONALE

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
SENAT

Sénat
Avenue du peuple Murundi
B.P. 114 GITEGA-BURUNDI
Tél : (257) 22 40 50 08 – 22 40 50 23
E-mail : cabinet@senat.bi – senat@senat.bi
Site web: www.senat.bi

Assemblée Nationale
B.P 120 Bujumbura-Burundi
Tél: (257) 22 26 70 11
Fax : (257) 22 26 70 12
E-mail : assemblenationale_burundi@yahoo.fr
Site web: www.assemblee.bi

- Kutambua na kuweka ramani ya makaburi ya halaiki na sehemu nyingine yoyote ilikozikwa miili bila ya kutambulika kisheria, kuchukua hatua zinazofaa ili kuvilinda, kuendelea na ufukuaji wa miili sawa na uwezekano kwa madhumuni ya kufanyiwa mazishi yenye heshima ili kuingilia kati baada ya udhihirisho wa ukweli;

- Maandalizi ya mahali maalum pa kuhifadhia mabaki ya miili ya wanadamu kabla ya kuzikwa kwa heshima (kipengele cha 6, aya ya 2);

**F. Kwa kuzingatia** matokeo ya shughuli ya Tume ya Ukweli na Maridhiano katika kutimiza majukumu yake ya kuchunguza na kubainisha ukweli kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na zile za kimataifa uliofanyika katika kipindi cha kuanzia Februari 26, 1885 hadi Desemba 04, 2008;

**G. Kwa kuzingatia** athari za mauaji ya 1972-1973 katika ngazi kadhaa, hasa ufutaji kabisa raia wa kabila ya Kihutu mashuleni na upande wa walimu vile vile, taratibu za kuwatenga Wahutu kwenye elimu, ufagiliwaji wao na kutengwa na jeshi, jinsi ambavyo Wahutu walinyanyaswa hasa na kutengwa katika sekta ya utawala wa kisiasa, uhamisho wa kulazimishwa kwa watu wengi wa kabila la kihutu, kiwewe na unyonge vilivyoendeshewa manusura na familia za waathirika, umasikini ambao ulisababishwa na uporaji wa mali zinazohamishika na zisizohamishika pia kama akaunti za benki;

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P. 120 BUJUMBURA
ASSEMBLEE NATIONALE

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P. 114 Gitega Tél 22 40 50 08
22 40 50 23
SENAT

H. **Kwa kuzingatia** jina ambalo limependekezwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano kwa uhalifu uliofanyika nchini Burundi mwaka 1972 -1973 kulingana na istilahi ya haki za binadamu na sheria za kimataifa;

I. **Kwa kuzingatia** kwamba ombi na utoaji msamaha ni msingi wa upatanisho wa kweli na kuweka mazingira muhimu na sahihi pia kwa amani kamilifu na maendeleo endelevu;

1. Bunge la Taifa na Baraza la seneti katika kikao cha kwa pamoja siku ya Jumatatu, Desemba 20, 2021 katika jumba la mikutano Kigobe **zinapasisha** magubiko ya ripoti ya maendeleo kihatua ya kupata ukweli kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliyoendeshwa nchini Burundi mwaka 1972-1973 ambayo imewasilishwa kikaoni na Tume ya Ukweli na Maridhiano;

2. Kikao cha Bunge na seneti kwa pamoja **kinapasisha** rasmi kwa dhati ripoti ya kufuzu iliyofikishiwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano siku hii ya tarehe 20 Desemba 2021;

3. Kikao cha Bunge na Baraza la Seneti kwa pamoja **kinapasisha** rasmi uhakikisho kamili ambao umewasilishwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano **kuthibitisha** kwamba ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu uliofanyika kote Burundi mwaka 1972-1973 kufuatia uchunguzi uliofanywa unadhihirisha mauaji ya kimbari dhidi ya raia wa kihutu wa Burundi;

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P 114 Gitega Tél 22 40 50 08
22 40 50 23
SENAT

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P. 120 BUJUMBURA
ASSEMBLEE NATIONALE

Sénat
Avenue du peuple Murundi
B.P. 114 GITEGA-BURUNDI
Tél : (257) 22 40 50 08 – 22 40 50 23
E-mail : cabinet@senat.bi – senat@senat.bi
Site web: www.senat.bi

Assemblée Nationale
B.P 120 Bujumbura-Burundi
Tél: (257) 22 26 70 11
Fax : (257) 22 26 70 12
E-mail : assemblenationale_burundi@yahoo.fr
Site web: www.assemblee.bi

4. Bunge na Baraza la Seneti zikijijumuisha na Kongamano maalum **zapasisha** rasmi kauli iliowasilishwa na Tume ya ukweli na Maridhiano mbele ya Bunge na Seneti kuthibitisha kwamba uhalifu dhidi ya binadamu uliendeshwa dhidi ya raia wa kihutu katika maeneo yote ya Taifa la Burundi;

5. Kikao cha Bunge na Seneti kwa pamoja **chapasisha** rasmi tamko zito ambalo limefikishwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano mbele ya Bunge na Baraza la Seneti kuthibitisha kwamba uhalifu dhidi ya binadamu uliendeshwa dhidi ya raia wa kitutsi kusini mwa nchi, hasa upande wa mwambao wa Ziwa la Tanganyika, katika wiki ya kwanza ya mlipuko wa mauaji ya mwaka 1972;

6. Kongamano la Bunge na Seneti **lapasisha** rasmi tangazo ambalo limewasilishwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano Bungeni kuthibitisha kwamba uhalifu dhidi ya binadamu uliendeshwa dhidi ya wananchi wa jamii ya Watwa, hasa katika mikoa ambayo sasa ni Muramvya na Mwaro;

7. Kikao cha Bunge na Seneti katika jumba la mikutano Kigobe **kinapasisha** rasmi kauli ambayo imetolewa na kuletwa mbele zake na Tume ya Ukweli na Maridhiano kuhitimisha kwamba hapakuwepo kamwe uhalifu wa kivita nchini Burundi mwaka 1972-1973;

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P. 120 BUJUMBURA
ASSEMBLEE NATIONALE

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P. 114 Gitega Tél 22 40 50 08
22 40 50 23
SENAT

Sénat
Avenue du peuple Murundi
B.P. 114 GITEGA-BURUNDI
Tél : (257) 22 40 50 08 – 22 40 50 23
E-mail : cabinet@senat.bi – senat@senat.bi
Site web: www.senat.bi

Assemblée Nationale
B.P 120 Bujumbura-Burundi
Tél: (257) 22 26 70 11
Fax : (257) 22 26 70 12
E-mail : assemblenationale_burundi@yahoo.fr
Site web: www.assemblee.bi

8. Kongamano la Bunge na Seneti **laitaka** Nchi ya Burundi kutambua kwa dhati na kisheria pia kuwa, mauaji ya kimbari yalifanyika dhidi ya raia wa kihutu wa Burundi mwaka 1972-1973;

9. Kikao maalum cha Bunge na Baraza la Seneti **kinazialika** taasisi husika kufanyia kazi upasishaji sheria ya ukumbusho ambayo itaundwa na kusisitizia ombi na utoaji wa msamaha ili kukuza upatanisho wa kitaifa;

10. Bunge na Seneti **zinaitaka** Nchi ya Burundi kuweka utaratibu wa kuwachukulia hatua za kisheria wale ambao wanadhaniwa kuwajibika na kukataa kuomba msamaha kwa makosa yaliyofanyika na kuwapa msamaha wa dhati wale ambao wanauomba ili wasije wakaponza mpango mzima wa maridhiano kwa ngazi ya kitaifa;

11. Kikao maalum cha Bunge na Baraza la Seneti **kinaalika** Nchi ya Burundi kuweka siku ya kitaifa ajili ya ukumbusho wa mauaji ya kimbari yaliyofanyika dhidi ya raia wa kihutu wa Burundi mnamo miaka ya 1972-1973;

12. Kongamano la Bunge na Seneti **linaialika** Nchi ya Burundi kuomba rasmi msamaha, kwa niaba ya Taifa la Burundi, kwa familia zote zilizofiwa mnamo 1972-1973 na kushiriki katika jitihada za ukarabati wa nyoyo za waathiriwa hasa kwa kuanzisha mpango maalum wa fidia za maadili, haswa kwa kuondoa jina chafu la "Bamenja" lililopewa familia za wahanga wasio na hatia;

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
B.P. 120 BUJUMBURA
ASSEMBLEE NATIONALE

REPUBLIQUE DU BURUNDI
Cabinet du Président
SENAT

Sénat
Avenue du peuple Murundi
B.P. 114 GITEGA-BURUNDI
Tél : (257) 22 40 50 08 – 22 40 50 23
E-mail : cabinet@senat.bi – senat@senat.bi
Site web: www.senat.bi

Assemblée Nationale
B.P 120 Bujumbura-Burundi
Tél: (257) 22 26 70 11
Fax : (257) 22 26 70 12
E-mail : assemblenationale_burundi@yahoo.fr
Site web: www.assemblee.bi

13. Bunge na Seneti vikijumuika na kikao cha kwa pamoja **zinaalika** Nchi ya Burundi kuitaka jumuiya ya kimataifa kusaidia kifedha harakati za shughuli ambazo zinaendeshwa na Tume ya Ukweli na Maridhiano;

14. Kongamano la Bunge na Baraza la Seneti **linaialika** Serikali ya Jamhuri ya Burundi kuutaka Ufalme wa Ubelgiji kuchukua jukumu lake kulingana na mgawanyiko wa jamii ambao ulitokana na utawala wake wa zamani nchini Burundi na sheria za madhehebu ambazo nchi hii iliweka juu ya Taifa la Burundi;

15. Bunge na Seneti zikijumuika na kikao cha kwa pamoja, **zinaiomba** Serikali ya Jamhuri ya Burundi kualika mashirika ya ushirikiano wa pande tofauti, hususan Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, pamoja na taratibu zinazohusishwa na mashirika haya ili kuhalalisha matokeo ya tafiti hizo ambazo zilifanyiwa kazi na Tume ya Ukweli na Maridhiano;

16. Kikao cha Bunge na Seneti kwa pamoja **kinaalika** Nchi ya Burundi kupatishia Tume ya Ukweli na Maridhiano jumba maalum yatakapohifadhiwa kwa muda mabaki ya binadamu na vitu vinginevyo ambavyo vilifukuliwa katika makaburi ya halaiki;

17. Kongamano la Bunge na Seneti kwa pamoja **laitaka** Tume ya Ukweli na Maridhiano kuandaa mikutano katika ngazi ya kitaifa na ile ya kimataifa kwa madhumuni ya kutangazia kote matokeo ya ripoti hii ya maendeleo kihatua, mwaka wa 2021;

18. Kikao cha Bunge la Taifa na Baraza la Seneti kwa pamoja kinazitaka Ofisi za Bunge na Seneti kuwasilisha tamko hili upande wa Taifa la Burundi.

**Imefanyika Bujumbura, Desemba 20, 2021**

| | |
|---|---|
| **SPIKA WA BARAZA LA SENETI** | **SPIKA WA BUNGE LA TAIFA** |
| **Mhe. Emmanuel SINZOHAGERA** | **Mhe. Gelase Daniel NDABIRABE** |